



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI

MSIMAMIZI WA UCHAGUZI

HALMASHAURI YA WILAYA YA BUSEGA

JIMBO LA BUSEGA



Kumb.Na.BDC/A.30/70/64

17 Oktoba, 2020

Yah: **TANGAZO LA KUTEULIWA KUFANYA SHUGHULI YA KUSIMAMIA
VITUO VYA KUPIGIA KURA UCHAGUZI MKUU 2020 JIMBO LA BUSEGA**


Kwa mujibu wa Kanuni ya 14 ya Kanuni za Uchaguzi wa Rais na Wabunge za mwaka 2020 na Kanuni ya 12 ya Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa (Uchaguzi wa Madiwani) za mwaka 2020, Msimamizi wa Uchaguzi atateua Wasimamizi wa Vituo, Wasimamizi Wasaididzi wa Vituo vya kupigia kura na Makarani waongozaji wapiga kura kwa idadi itakavyoeleekzwa na Tume ili kufanikisha upigaji kura.


Kwa mamlaka niliyopewa nimewateuwa Wasimamizi wa vituo 325, Wasimamizi wasaidizi 650 na Makarani waongozaji 325 kusimamia vituo 325 vya kupigia kura ndani ya Jimbo la Busega. Pia nimeteua wasimamizi wa vituo wa akiba 30 na makarani waongozaji wapiga kura wa akiba 30.

Wateule wote mnatakiwa kuhudhuria mafunzo kabla ya kuanza kazi. Mafunzo ya Makarani waongozaji yatakuwa tarehe 24/10/2020 na mafunzo ya wasimamizi wa vituo na wasimamizi wasaidizi wa vituo vya kupigia kura yatakuwa tarehe 25-26/10/2020.

Aidha, kwa kata za Lamadi, Mkula, Lutubiga, Kalemela, Imalamate, Ngasamo na Malili mafunzo yatafanyika katika Ukumbi wa shule ya awali Lukungu na kwa kata za Nyashimo, Shigala, Igalukilo, Nyaluhande, Kabita, Kiloleli, Mwamanyili na Badugu Mafunzo yatafanyika katika ukumbi wa shule ya Sekondari Bulima.

Pamoja na Tangazo hili Majina yaliyoteuliwa yameambatishwa.


Anderson Njiginya Kabuko
Msimamizi wa Uchaguzi
JIMBO LA BUSEGA



Sanduku la Posta 157, Busega; Simiyu; simu-+255 (028) 2981193, Nukushi- +255 (028)2981194
Barua pepe: ded@busegadc.go.tz na Tovuti: www.busegadc.go.tz